

HALMASHAURI YA MJI WA MBULU

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu Na. +255 272 2533331
Fax 255 272 2533330
Email: td.mbulutc.go.tz



Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Mji wa Mbulu,
S.L.P. 164
Mbulu/ Manyara

Kumb.Na.MTC/TD/RS/13/97

11/11/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu anawatangazia Nafasi za Kazi na anakaribisha maombi ya Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza Nafasi ya kazi kama ifuatavyo:-

1.1 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 1).

Nafasi hii ni kwa ajili ya Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au chuo chochote kinachotambulika na serikali.

1.1.2 MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na mtendaji mkuu wa Serikali ya kijiji,
- Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na Msimamizi wa utawala bora katika kijiji,
- Katibu wa mikutano wa kamati zote za Kijiji,

- Kutafsiri na kusimamia sheria na taratibu zote za kwenye Kijiji,
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli zote za kwenye eneo lake,
- Kuhamisisha wananchi katika kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo,
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu pamoja na nyaraka mbalimbali za kijiji,
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogondogo,
- Kupokea, kusikiliza na kutatua kero na migogoro mbalimbali ya wananchi.

1.1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B** kwa mwezi

MASHARTI YA JUMLA.

- i. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayo jitosheleza (Detailed C.V)
- iii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (Passport Size) na kila picha iandikwe jina nyuma.
- iv. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- v. Uwasilishaji wa taarifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- vi. **Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 02 Desemba, 2020 saa 9.30**

viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na kuwasilishwa Masjala bayana ya Halmashauri ya Mji iliyoko eneo la Ujenzi au kwa njia ya posta kwa kutumia anwani ifuatayo.

**MKURUGENZI WA MJI,
HALMASHAURI YA MJI WA MBULU,
S.L.P. 164,
MBULU.**

AU

**TOWN DIRECTOR,
MBULU TOWN COUNCIL,
P.O.Box 164,
MBULU.**

**ANNA P. MBOGO
MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI
MBULU.**